

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ILIYOREKEBISHWA

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 4, 2021. Kampuni imerekebisha maazimio kwenye Taarifa ya Mkutano Mkuu na imeongeza ajenda nyingine. Kwasasa Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:

- 21.1 MATANGAZO NA AKIDI
- 21.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 21.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2020
- 21.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 20 WA WANAHISA
- 21.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020
- 21.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020
- 21.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI
- 21.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI
- 21.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI
- 21.10 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2021
- 21.11 MENGINEYO

## MAELEZO MUHIMU

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayerusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua wakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebisha. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 3 Juni 2021.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za uwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB ([www.nmbbank.co.tz](http://www.nmbbank.co.tz)).
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 137 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 68.5 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2020.

## Tarehe za kuzingatia:

Tarehe ya tangazo:	14 Mei 2021
Hisa kuuzwa pamoja na gawio :	14 Mei 2021
Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :	2 Juni 2021
Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:	3 Juni 2021 nakuendelea
Daftari la wanahisa kufungwa:	7 Juni 2021
Malipo ya gawio kwa wanahisa:	kuanzia tarehe 16 Juni 2021

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,



Lilian R. Komwihangiro  
Katibu wa Kampuni  
7 Mei 2021